



**OFISI YA RAIS TAWALA ZAMIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
CHUNYA**



Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na: CDC/F.20/62/VOL II/27

Tarehe: 21/06/2022

**MWALIKO WA ZABUNI  
ZABUNI NA. LGA/075/2022/2023/NS/01  
UTOAJI WA HUDUMA YA USAFI  
HOSPITALI YA WILAYA YA CHUNYA**


1. Halmashauri ya Wilaya ya Chunya inatoa mwaliko wa zabuni ya huduma ya usafi kwa vikundi vilivyosajiriwa au kampuni zote zenye sifa ya kutoa huduma ya usafi ,kuanzia mwezi agosti 2022 hadi juni 2023 kwa mkataba ambao unatolewa na mwaliko wa zabuni hii
2. Unakaribishwa kuleta zabuni yako ya bei kwaajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelekezwa kwenye maelekezo ya mahitaji na bei kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya II.
3. Eneo la huduma litakuwa mazingira yote ya Hospitali ya Wilaya ya Chunya.Huduma inapaswa kuanza kutolewa kuanzia agosti ,2022 hadi juni 2023 baada ya kukubaliwa kwa zabuni ya utoaji wa HUDUMA YA USAFI.
4. Mtoa huduma (MH) lazima aambatanishe kwenye kotesheni yake nyaraka zifuatazo
  - i. Bei ya kotesheni iliyojazwa kikamilifu na kutiwa sahihi kulingana na maelezo ya mahitaji.
  - ii. Leseni halali ya biashara.
  - iii. VAT halali na cheti cha TIN.
  - iv. Taarifa za kifedha (Bank Statement) ya hivi karibuni miezi miwili.
  - v. Orodha ya mikataba ambayo mtoa huduma amewahi kufanya hivi karibuni inayofanana na huduma hii isiyopungua miwili.Mtoa huduma lazima aonyeshe

*majina na anwani za mwajiri aliyempa kazi hiyo kwaajili ya uthibitisho.*

- vi. Mwombaji awe na vibarua wakutosha kufanya kazi ya usafi kwa wakati.
5. Kampuni/kikundi ambacho wanasifa na uwezo wa kutoa huduma ya usafi Hospitali ya Wilaya ya Chunya ,wafike Ofisi ya kitengo cha Manunuzi/Ugavi chumba namba 4 kuchukua fomu za mchanganuo wa kazi na kotesheni za bei(schedule of requirements/service kwaajili ya kazi husika ambao unatolewa bure.
6. Maombi yawe na maelezo ya kina na viambatanisho muhimu,yafungwe vizuri kwenye bahasha na kuwekwa lakiri na kutumwa kwa :-

**KATIBU BODI YA ZABUNI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S.L.P.73  
CHUNYA.**

7. Kwa wale wote watakao leta maombi yao kwa mkono barua zote zipelekwe ofisi NAMBA 4 (NNE) KITENGO CHA UGAVI Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.00 Alasiri siku za kazi (Jumatatu hadi Ijumaa) na hakikisha unajiorodhesha kwenye rejista ya mapokezi ya zabuni husika.
8. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya FAX, Telefax na Telegraphic system hayatapokelewa na kufunguliwa siku ya Ufunguzi.
9. Mwisho wa kupokea maombi ni **JUMATANO TAREHE 29 JUNI 2022** saa 6.00 mchana na zabuni zote kufunguliwa **JUMATANO 29 JUNI 2022** saa 6.30 mchana katika ukumbi wa mikutano Sapanjo.Waombaji mnakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni kwa gharama zenu.

  
Cuthbert Mwinuka  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
CHUNYA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHUNYA**